



# Je, unataka kubakia nyumbani na kuondowa fujo?

AMRI YA KUZUIA FUJO NYUMBANI  
(APPREHENDED DOMESTIC VIOLENCE ORDER)

## Amri ya kuzuia fujo nyumbani maanake nini?

Kupatikana kwa amri ya kuzuia fujo nyumbani (ADVO) inakuruhusu wewe ubakie nyumbani na kumtoa anayefanya fujo.

Amri ya kuzuia fujo nyumbani inakulinda wewe na inaondoa na kumzia yule mtu anayeleta fujo katika nyumba.

## Unahitaji amri hii?

Kabla ya kuomba amri ya kuzuia fujo nyumbani, kuna maswali mbalimbali ingefaa ujiulize:

1. Utakaa salama ukibakia peke yako nyumbani?
2. Utaogopa kama mfanyakaji fujo anafahamu mahali unapoishi?
3. Unapenda kubakia nyumbani na kutaka mtu anayeleta fujo ahamishwe?
4. Una watoto? Unafikiri watakuwa na furaha zaidi wakibakia nyumbani na wewe?
5. Je utaweza kulipa gharama za nyumba?

## Utapataje amri ya kuzuia fujo nyumbani?

Hakimu anaweza kutoa amri ya kuzuia fujo nyumbani kama umesitisiza katika ombi lako.

Ukitaka kuomba amri hii ni lazima uzungumze na wakili, ama mtumishi wa mahakamani, ama askari.

Ni vizuri kupata amri hii kwa sababu amri inaweza kutumiwa na askari kuzuia na kusimamisha fujo.

## Nini ni muhimu mahakamani wakati wa kuamua amri ya kuzuia fujo nyumbani?

Mahakama huchunguza mambo mbalimbali kabla ya kuamua utoaji wa amri ya kuzuia fujo nyumbani. Kwa mfano:

1. Usalama wako na usalama wa watoto wanaoishi nyumbani.
2. Shida zote zitakazosababishwa na kutoa au kutotoa amri, hasa kwako wewe na watoto wanaoishi katika nyumba.
3. Mahitaji ya wahusika wote, hasa mahitaji binafsi na ya watoto pia.
4. Jambo lolote lianalohusika na amri ya kuzuia fujo nyumbani.

Usisahau kutoa taarifa kwenye kituo cha polisi kuhusu uvunjaji wowote wa amri ya kuzuia fujo nyumbani.

## Tafadhal! Usisahau kufikiria Usalama Wako wakati wote.

### Je, utapata msaada wapi?

Polisi/Gari la wagonjwa 000

Simu ya kufahamisha fujo nyumbani (Domestic Violence Line) 1800 656 463

Kituo cha Kipeo Kinachotokana na Ubakaji cha NSW (NSW Rape Crisis Centre) 1800 424 017

Nambari ya Ulinzi wa Watoto (FACS Child Protection Helpline) 13 21 11

Huduma za Kisheria kwa Wanawake wa NSW (Women's Legal Services NSW)

Sydney (02) 9749 5533 Nje ya Sydney 1800 801 501

Huduma zinazohusika na fujo za nyumbani (Domestic Violence Advocacy Service)

Sydney (02) 8745 6999 Nje ya Sydney 1800 810 784

Sauti ya Wanawake Wahamiaji (Immigrant Women's Speakout) (02) 9635 8022

Nambari ya Kusaidia Watoto (Kids Helpline) 1800 551 800

Kituo cha Msaada wa Kifedha Centrelink (Financial Assistance Centrelink) 13 61 50

Huduma za Tafsiri na Fasiri (TIS) 13 14 50

Unaweza kupata nambari ya simu ya Kituo cha Polisi au Mahakama ya Mtaa yanayopatikana karibu na mahali unapoishi kwenye kurasa nyeupe za kwanza katika kitabu cha nambari za simu



Family & Community Services  
Community Services